JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI

# Jarida La Mtandaoni

Toleo la Sita, 2021



# MAWAZIRI WAKETI KUWEKA MAMBO SAWA, NI KUHUSU MAAGIZO YA RAIS YA ONLINE TV



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Dkt. Faustine Ndugulile (katikati) akizungumza katika kikao cha pamoja na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa (kushoto) cha kujadili hoja zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya Sekta hizo ya kisera, kisheria na kikanuni kwenye masuala ya mawasiliano na utangazaji nchini kilichofanyika jijini Dodoma, Kulia ni Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Kundo Mathew.

**Na Faraja Mpina**

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Faustine Ndugulile na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wamefanya kikao cha pamoja na Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu pamoja na wataalamu kujadili hoja mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya Sekta ya Mawasiliano na Utangazaji nchini hasa wakiangazia suala la Online TV katika vipengele vya usajili, kanuni, sheria, miongozo pamoja na tozo.

Kikao hicho kimefanyika tarehe 14.04.2021 Jijini Dodoma kikiwa ni utekelezaji wa maelekezo yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan katika hotuba yake wakati akiwaapisha Makatibu Wakuu, Manaibu Katibu Wakuu na Wakuu wa Taasisi kuhusu kufanya marekebisho ya kanuni na sheria zinazosimamia vyombo vya habari nchini hususani Televisheni Mtandao (Online TV)

Miongoni mwa maazimio yaliyoafikiwa na pande zote mbili ni pamoja na kuangaliwa upya muundo mzima wa uwajibikaji wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa Wizara zote mbili pasipo kuathiri utekelezaji wa majukumu ya mamlaka hiyo katika Sekta ya Mawasiliano na Utangazaji nchini.

Aidha, mawaziri hao walikubaliana kuzipitia upya kanuni, sheria na miongozo mbalimbali kuhusu Online TV ikiwa ni pamoja na kuweka mifumo rafiki ya usajili na malipo kuangalia uwezekano wa kupunguza tozo na kufanya uchambuzi yakinifu wa nani anatakiwa kulipia kuendena na matumizi husika.

Katika hatua nyingine TCRA ilipewa maelekezo ya kuongeza utoaji wa elimu kwa umma kuhusu usajili, kanuni, sheria na taratibu zote za Online TV ili ziwe wazi kwa wananchi na elimu hiyo iambatane na elimu ya matumizi sahihi ya mtandao kwa lengo la kuongeza uwazi na uwajibikaji wa pamoja.

Pamoja na mambo mengine mawaziri hao walipitia hoja mbalimbali zinazotakiwa kufanyiwa mapitio na maboresho ikiwa ni pamoja na chaneli za runinga zinazotakiwa kuonekana katika visimbuzi bila malipo (FTA), kanuni za maudhui na utoaji wa




Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Kundo Mathew akizungumza katika kikao cha cha kujadili hoja zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya kisera, kisheria na kikanuni kwenye masuala ya mawasiliano na utangazaji nchini kilichofanyika jijini Dodoma baina ya Wizara hiyo na Wizara Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo anayefuata ni Waziri wake Mhe. Dkt Faustine Ndugulile, akifuatiwa na Wazi Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa na kushoto ni Naibu wake Mhe. Pauline Gekul.

Mawaziri hao kwa pamoja na watendaji wao wakuu wamejipanga kuhakikisha Sekta wanazozisimamia hasa katika maeneo ambayo yana muingiliano katika utendaji wao yanafanyiwa maboresho makubwa kuendana na hali halisi ya sasa ya kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na kuhakikisha malalamiko ya wananchi yanafanyiwa kazi na wao kama watendaji wanazungumza lugha moja kwa manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Wajumbe waliohudhuria kikao hicho ni pamoja na Naibu Waziri wa Wizara ya Mawasiliano na Tekbnolojia ya Habari Mhe. Mhandisi Kundo Mathew, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Zainab Chaula na Naibu wake Dkt. Jim Yonazi, Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo Mhe. Pauline Gekul na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Hasaan Abbas.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Dkt. Hassan Abbas (kushoto) akizungumza leo katika kikao cha Mawaziri wa Wizara hiyo na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari cha kujadili hoja zinazohusu utekelezaji wa majukumu ya Sekta hizo ya kisera, kisheria na kikanuni kwenye masuala ya mawasiliano nchini kilichofanyika jijini Dodoma.Kulia ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Zainab Chaula.
Kikao hicho kimefanyika kufuatia maelekezo yaliyotolewa hivi karibuni na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kutaka kufanyika marekebisho ya Sheria na Kanuni zinazosimamia Vyombo vya Habari hapa nchini hususan Televishen Mtandao (Online TV).

# DKT. NDUGULILE AITAKA TCRA KUELIMISHA UMMA NA KUBORESHA MIFUMO YA MALALAMIKO



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile akizungumza katika kikao chake na Wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo cha kujadili taarifa za mapato na matumizi na utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 katika ukumbi wa Hazina, Dodoma.

**Na Faraja Mpina**

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Dkt. Faustine Ndugulile ameiagiza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kushirikiana na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC) kuboresha vitengo vyao vya mawasiliano ili kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma kuhusu matumizi sahihi ya huduma za mawasiliano kwa kuzingatia haki na wajibu pamoja na matumizi sahihi ya simu janja na mtandao.

Dkt. Ndugulile amezungumza hayo mbele ya waandishi wa habari baada ya kikao chake cha kazi cha Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo cha kujadili na kufanya mapitio ya taarifa za mapato na matumizi za taasisi hizo kwa robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 Kilichofanyika katika Ukumbi wa Hazina jijini Dodoma.

Aidha Dkt. Ndugulile ameziagiza taasisi hizo kuboresha mifumo ya wananchi kutolea malalamiko yanayohusu huduma za mawasiliano na kushughulikia malalamiko hayo kwa wakati na taarifa ya malalamiko hayo itakuwa ni ajenda ya kudumu katika vikao vya kila robo mwaka baina ya Wizara hiyo na taasisi zake.

Ameongeza kuwa elimu kwa umma ikitolewa kwa kiwango kinachojitosheleza kitapunguza baadhi ya malalamiko ya wananchi kwa mfano malalamiko ya vifurushi vya data kuisha haraka ambapo kwa namna moja ama nyingine inasababishwa na settings za simu janja kuruhusu programu zake kujiboresha zenyewe (automatic Updating).

“Kuna mambo ambayo ni muhimu wananchi kuyafahamu kwa mfano matumizi makubwa ya data yanayosababishwa na settings za simu janja ambazo zinaruhusu baadhi ya programu kujiboresha zenyewe nazo zinachangia vifurushi vya data kuisha haraka”, alizungumza Dkt. Ndugulile

Aliongeza kuwa Serikali inatengeneza mazingira wezeshi ya kuhakikisha mawasiliano yanafika kwa wananchi wote lakini kumekuwa na changamoto ya baadhi ya watu kutokuwa na matumizi sahihi ya huduma hii, hivyo wananchi wanahitaji kuelemishwa ili kuhakikisha wanajua wajibu wao na haki zao na kuwa na matumizi sahihi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Akizungumzia kikao cha Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo cha mapato na matumizi Dkt. Ndugulile amesema kuwa lengo ni kusimamia nidhamu na matumizi ya fedha za taasisi hizo badala ya kusubiri mpaka mwisho wa mwaka CAG aje kuhoji.

“Sisi kama Wizara tunajipanga kuhakikisha fedha zinazopatikana zinaelekezwa katika kutekeleza majukumu ya msingi ya Wizara na taasisi zake ikiwa ni pamoja na kwenda kutekeleza miradi ya maendeleo.

Dkt. Ndugulile amezielekeza taasisi zilizo chini ya Wizara yake kutolea ufafanuzi maeneo ambayo yaliguswa katika taarifa ya CAG na kama kuna hoja zozote ziliyojitokeza zijibiwe kikamilifu na kuwasilishwa ndani ya wiki ijayo na taasisi ambazo hazikuwasilisha hesabu zao kwa CAG watoe maelezo kwa nini hawakuziwasilisha kwa mujibu wa taratibu za Serikali

Naye Naibu Waziri wa Wizara hiyo Mhe. Kundo Mathew amezitaka taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo kufanya kazi kwa ushirikiano kwa kutambua kuwa Wizara inayowasimamia ipo makini kuhakikisha taasisi hizo zinatimiza wajibu wake wa kuhudumia wananchi na yeye kama msaidizi wa Waziri mwenye dhamana atashirikiana na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo na Naibu wake kuhakikisha kuwa Wizara na taasisi zake zinafanya kazi zenye ubora na kwa wakati ikiwa ni pamoja na kuandaa taarifa zinazojitosheleza bila kusubiri maelekezo.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Zainab Chaula, Naibu wake Dkt Jim Yonazi, Wakuu wa taasisi za Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Shirika la Mawasiliano Tanzania (TTCL), Tume ya Taifa ya Tehama (ICTC), Shirika la Posta Tanzania (TPC), Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) na Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC), Menejimenti ya Wizara pamoja na baadhi ya watendaji wa taasisi zake.



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile (wa pili kushoto) akizungumza katika kikao chake na Wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo cha kujadili taarifa za mapato na matumizi na utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 katika ukumbi wa Hazina, Dodoma. Wa pili kulia ni Naibu wake Mhandisi Kundo Mathew kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo Dkt. Zainab Chaula na kulia ni Naibu wake Dkt. Jim Yonazi.



Baadhi ya wajumbe wa kikao cha Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dkt. Faustine Ndugulile na Wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo cha kujadili taarifa za mapato na matumizi na utekelezaji wa majukumu kwa kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2020/2021 katika ukumbi wa Hazina, Dodoma.

**Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**
**Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**
**S.L.P. 677,40470 Dodoma, Tanzania**
**Barua pepe: ps@mawasiliano.go.tz**
**Tovuti: www.mawasiliano.go.tz**
**Instagram: Wizaramth**